

HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha
Telegram: Meru
Simu: (+ 255) 027 254-1112
Faksi: (+ 255) 027 254-1112
Barua pepe: merudc@yahoo.com
Tovuti : www.merudc.go.tz



Ukumbi wa Wilaya,
S.L.P 462,
USA RIVER

18.04.2017

TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Wilaya ya Meru inawatangazia zabuni wananchi wote wenye uwezo na sifa ya kukusanya ushuru/mapato ya Halmashauri na usafishaji wa mazingira kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 kama ifuatavyo:

(A) UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO:

NA.	AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI	ENEO LA KUKUSANYA USHURU
1.	Ushuru wa choo na soko - Msorongo	LGA/001/2017/2018/NC/01	Soko la Msorongo
2.	Ushuru wa soko na choo - Tengeru	LGA/001/2017/2018/NC/02	Soko la Tengeru
3.	Ushuru wa choo na Kituo cha Mabasi Tengeru	LGA/001/2017/2018/NC/03	Kituo cha mabasi Tengeru
4.	Ushuru wa soko - Usa River	LGA/001/2017/2018/NC/04	Soko la Usa-River
5.	Ushuru wa soko na mnada - Kikatiti	LGA/001/2017/2018/NC/05	Soko la Kikatiti
6.	Ushuru wa madini ya ujenzi - King'ori na Mlima Siyoni	LGA/001/2017/2018/NC/06	King'ori na Mlima Siyoni
7.	Ushuru wa soko - Kolila	LGA/001/2017/2018/NC/07	Soko la Kolila
8.	Ushuru wa soko - King'ori	LGA/001/2017/2018/NC/08	Soko la King'ori
9.	Ushuru wa soko - Leguruki	LGA/001/2017/2018/NC/09	Soko la Leguruki
10.	Ushuru wa soko na mnada - Ngarenanyuki	LGA/001/2017/2018/NC/10	Soko na mnada wa Ngarenanyuki
11.	Ushuru wa Maegesho	LGA/001/2017/2018/NC/11	Usa River
12.	Ushuru wa soko na Mnada wa Shambarai Burka	LGA/001/2017/2018/NC/12	Soko na Mnada wa Shambarai Burka
13.	Ushuru wa Kituo cha Mabasi -Mbuguni	LGA/001/2017/2018/NC/13	Kituo cha mabasi - Mbuguni
14.	Ushuru wa soko - Mbuguni	LGA/001/2017/2018/NC/14	Soko la Mbuguni
15.	Ushuru wa Mazao	LGA/001/2017/2018/NC/15	Tarafa za Poli, Mbuguni na King'ori

(B) UWAKALA WA USAFISHAJI WA MAZINGIRA:

NA.	AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI	ENEO LA USAFISHAJI
1.	Usafishaji wa mazingira	LGA/001/2017/2018/NC/16	Kata ya Ambureni, Akheri, Seela Sing'isi na Poli
2.	Usafishaji wa mazingira	LGA/001/2017/2018/NC/17	Mamlaka ya mji mdogo wa Usa River, Kata ya Nkoaranga (kijiji cha Nshupu) na kata ya Nkoanekoli (kitongoji cha Kwa Mangusha)
3.	Usafishaji wa mazingira	LGA/001/2017/2018/NC/18	Kata ya Imbaseni na Maji ya Chai
4.	Usafishaji wa mazingira	LGA/001/2017/2018/NC/19	Kata ya Kikatiti na Malula

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

1. Mwombaji lazima awe na leseni hai na stahili ya biashara, TIN/VAT, Hati ya Usajili wa jina la biashara na ofisi inayotambulika.
2. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha, athibitisha kwa kuambatanisha 'Bank Statement' ya miezi mitatu (3) iliyopita kutoka tarehe aliyoomba zabuni au 'Audited Financial Statement' ya miaka miwili ya karibuni.
3. Mwombaji aambatanishe "Power of Attorney" kwa zabuni husika,
4. Ada ya maombi ya zabuni ni Tshs. 50,000/= (Shilingi Elfu hamsini tu), ambapo mwombaji atatakiwa kufika Halmashauri kwa ajili ya kupewa Ankara kisha malipo yatafanyika kupitia akaunti ya Halmashauri ya Meru iliyoko katika Benki ya NMB, tawi la Clock Tower, akaunti ya Jumla ya Halmashauri ya Meru, Account No. 40801200330. Malipo yaliyotolewa kama ada ya maombi ya zabuni hayatarudishwa.
5. Mwombaji awe na vifaa vya kutosha kumudu vyema zabuni aliyoomba.
6. Mwombaji awe tayari kulipa dhamana ya zabuni ya kiwango cha miezi miwili (2) cha maoteo kwa mwezi na awe na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika na wanaotambulika, kabla ya kusaini mkataba.
7. Awe tayari kutumia viwango vilivyowekwa katika Sheria ndogo za Halmashauri vya ukusanyaji wa mapato.
8. Mzabuni atakayeteuliwa atatumia mashine za kielektroniki (POS) kukusanyia ushuru wa Halmashauri
9. Maombi yawe na maelezo ya kina na viambatisho husika (kama Company Profile, n.k) na kutumwa kwa:

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,
Halmashauri ya Wilaya ya Meru,
S.L.P 462,
Usa River.**

10. Maombi yatakayoletwa kwa njia ya Fax, Telefax, na Telegraphic System na yatakayochelewa hayatapokelewa na hayatafunguliwa siku ya ufunguzi.
11. Kabrasha la zabuni na maelezo mengine yanapatikana katika ofisi za Makao makuu ya Halmashauri ya Meru, Usa River, katika ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Chumba Na.36, Ghorofa ya kwanza, kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri (siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu za kitaifa)
12. Maombi ya Zabuni zote yawasilishwe katika Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni wa Halmashauri, Makao Makuu ya Halmashauri ya Meru. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni ***Ijumaa, tarehe 12/05/2017, saa nne (4) asubuhi***. Waombaji au wawakilishi wao, wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika siku hiyo ya tarehe ***12/05/2017 saa nne (4) asubuhi*** katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.

Christopher J. Kazeri
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA MERU